Pia napenda kuchukua fursa hii kuutarifu umma kuwa EWURA imefungua ofisi nyingine jijini Mbeya ambayo ilizinduliwa tarehe 28 Septemba 2017 kwa ajili ya kuhudumia mikoa saba ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini; Mbeya, Songwe, Rukwa, Katavi, Iringa, Njombe na Ruvuma.

Toleo hili lina habari nyingi za kuvutia kutoka sekta ndogo tatu ambazo EWURA inazidhibiti za nishati; Petroli; Umeme na Gesi Asilia na Sekta moja ya Maji; Maji na Usafi wa Mazingira; zilizotokana na shughuli za udhibiti zilizofanyika kati ya Julai na Septemba 2017.

Katika kipindi hiki, EWURA imefanya maamuzi mbalimbali ya kiudhibiti ambayo baadhi yake, yamechapishwa katika toleo hili, ambalo linachapishwa katika kutekeleza kifungu cha 6(e) cha Sheria ya EWURA Sura Na. 414 ya Sheria za Tanzania.

Kipengele cha 6(e) kinasema kwamba ni wajibu wa Mamlaka kuhakikisha inaboresha ustawi wa jamii ya Watanzania kwa kuimarisha elimu kwa umma, ufahamu na uelewa wa sekta zinazodhibitiwa ikiwa pamoja na; haki na wajibu wa walaji na watoa huduma wa sekta zinazodhibitiwa; Njia za kutatua migogoro na kusikiliza malalamiko, kazi na shughuli za mamlaka kwa ujumla.

Katika toleo hili shughuli ambazo zimepewa kipaumbele kuchapishwa ni pamoja na RC Arusha kuihakikishia EWURA *sapoti*, Jinsi Mdhambi anavyoheshimu mazingira, Wawakilishi wa Z'bar waitembelea EWURA na habari zingine kemkemu za kuvutia.

Wote mnakaribishwa!



Titus Kaguho

RC Arusha aihakikishia EWURA sapoti ofisi mpya ya Kanda ya Kaskazini

Na Titus Kaguo

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imefungua Ofisi ya Kanda ya Kaskazini, mijini Arusha; ambayo ni mwendelezo wa Mamlaka kufungua Ofisi zake za Kanda nchini katika juhudi za kusogeza huduma zake karibu na wananchi.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mheshimiwa Mrisho Gambo ameunga mkono hatua hii kwa kuihakikishia EWURA kuwa atatoa ushikiano wa hali ya juu katika usimamizi wa Ofisi hiyo, ikiwemo kuhakikisha kuwa masuala yote yanayohusu utekelezaji wa majukumu ya EWURA ikiwemo kanuni zinazoongoza utoaji wa huduma,

zinafuatwa na wadau wote wanaopokea huduma hizo katika mkoa wake.

Mhe. Mkuu wa Mkoa alitoa kauli hiyo hivi karibuni wakati wa uzinduzi wa wa Ofisi ya EWURA, Kanda ya Kaskazini; Ofisi ambayo itahudumua mikoa minne ya Arusha, Manyara, Kilimanjaro na Tanga.

Gambo aliishukuru EWURA kwa kuamua kuifanya Arusha kuwa makao makuu ya Ofisi yake kwa Kanda ya Kaskazini; kwa kusema: “EWURA ingeweza kuchagua kuweka makao makuu katika mikoa mingine ya Kanda hii. Niwahakikishie



Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mhe. Mrisho Gambo (katikati) akikata utepe wakati wa uzinduzi wa ofisi mpya za EWURA kwa Kanda ya Kaskazini tarehe 5 Agosti 2017. Kushoto ni Mwenyekiti wa Bodi ya EWURA Mha., Prof. Jamidu Katima na kulia ni Meneja wa EWURA wa Kanda ya Kaskazini Bi. Kapwete Leah John.



Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mhe. Mrisho Gambo, akiwa katika picha ya pamoja na Wajumbe wa Bodi, Menejenti ya EWURA wakati wa uzinduzi wa ofisi mpya ya Kanda ya Kaskazini jijini Arusha, Agosti 2017.

tu kwamba chaguo lenu kwa Arusha kuwa makao makuu ya Kanda, limeniongezea ari na nitawajibika kuhakikisha kuwa mnaendesha shughuli zenu kwa ushirikiano mkubwa kutoka kwangu mimi kama Mkuu wa Mkoa”.

Aidha, Mhe. RC alieleza kuwa, kwa muda mrefu watumiaji wa huduma za EWURA wamekua wakisumbuka kuzifuata huduma hizo mkoani Dar es Salaam ambapo ndio yalipo makao makuu ya Mamlaka kwa sasa, jambo ambalo limekua likiwapa usumbufu mkubwa kutokana na kupoteza muda mwingi na gharama kwa kusafiri kwenda Dar es Salaam; hali ambayo kwa sasa itakua tofauti kwa kuwa huduma zote zilizokuwa zinafuatwa Dar es Salaam, sasa zitapatikana hapa Arusha na kuongeza kuwa wale wote wanaohitaji huduma za Mamlaka watazipata Arusha na watatumia muda na gharama zao kufanya shughuli nyingine za kimaendelo.

Awali, Mwneyekiti wa bodi ya Wakurugenzi ya EWURA, Mhandisi, Prof. Jamidu Katima alieleza kuwa ana imani na mategemeo kuwa, Ofisi ya

Mkuu wa Mkoa itatoa ushirikiano wa hali ya juu ili kuifanya Ofisi hiyo ya Kanda kufanya shughuli zake katika viwango vinavyostahili, kwa uhakika na kwa usalama.

“Ni matarajio yetu kuwa kwa kufungua Ofisi hii hapa Arusha, watumiaji wa huduma zetu kwa Kanda ya Kaskazini watapata huduma bora na kwa urahisi zaidi; Na nitumie fursa hii kuwakaribisha walaji na watumiaji wote wa huduma zetu kuwasilisha mahitaji yao katika Ofisi yetuhii, ili kupata uamuzi wa masuala yao haraka wiwezekanavyo,” alisema Mhandisi. Prof. Katima.

Ofisi ya Kanda ya Arusha ni ya pili kuanzishwa, ikitanguliwa na ile ya Kanda ya Ziwa iliyofunguliwa mwaka 2015, iliyopo Mwanza ambayo inahudima mikoa ya Mwanza, Kagera, Mara, Shinyanga na Simiyu; na vilevile, EWURA iko mbioni kufungua Ofisi nyingine ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, itakayokuwa Mbeya; ambayo itatoa huduma kwa mikoa ya Iringa, Njombe, Mbeya, Songwe, Rukwa, Katavi and Ruvuma.

Udhibiti wa Nishati, Maji na Utunzaji wa Mazingira

Na Tobietha Makafu

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji ni mamlaka huru ya udhibiti, iliyoanzishwa na sheria ya EWURA sura namba 414 ya sheria ya Tanzania, kwaajili ya kudhibiti kiufundi na kiuchumi sekta ya nishati, inayohusisha sekta ndogo ya umeme, Mafuta aina ya petroli, gesi asilia na maji kwa Tanzania.

EWURA inawajibwa wa kuhakikisha shughuli zote zinazodhibitiwa, zinahifadhi na kutunza mazingira kwaajili ya kulinda afya, usalama na mazingira ya watoa huduma, wateja wao na wananchi walio karibu.

Meneja wa Mawasiliano na Uhusiano EWURA Bw. Titus Kaguho alisema, katika udhibiti wa sekta ya umeme EWURA inahakikisha mazingira yanatunzwa kwa kutoa leseni ya uzalishaji umeme kwa mradi ambao umepata kibali cha Mazingira kutoka katika Baraza la Taifa la Mazingira NEMC, ili kuhakikisha mradi huo hauna athari zozote kwa mazingira.

Aliongeza na kusema kuwa EWURA imekua ikifanya ukaguzi ili kudhibiti taka zitokanazo na shughuli mbalimbali za uzalishaji umeme, mfano kukagua uteketezaji wa dizeli chafu inayozalishwa baada ya kuzalisha umeme wa mafuta ili kuondoa athari kwa mazingira, pia kuhakikisha hakuna kelele, vumbi na taka zingine zitakazoathiri, afya na usalama wa viumbe hai na mimea katika eneo hilo.

Akizungumzia sekta ya mafuta aina ya petroli, Bw. Kaguho alisema, kuna kanuni mbalimbali za udhibiti wa kiufundi zimewekwa ili kuhakikisha zinalinda afya, usalama, mazingira, ubora na hatari zote zinazoweza kutokea kama moto, magonjwa mbalimbali pamoja na kulinda mafuta

yasitiririke kwenda kwenye vyanzo vya maji na kuathiri shughuli za kilimo.

“Kanuni za sekta ya mafuta zinahakikisha EWURA inatoa leseni ya biashara ya mafuta yenye miundombinu ya usafirishaji na utunzaji wa petroli unaokidhi viwango vya kimataifa na TBS. EWURA imehakikisha kila kituo cha mafuta kina chemba ya kutenganisha mafuta na maji ili pindi mafuta yanapomwagika na kuchanganyika na maji yaweze kutenganishwa na kuhifadhiwa au kuteketezwa kwa usahihi”

Kwa upande wa gesi asilia Bw. Kaguho alisema. EWURA imekua mstari wa mbele kuhakikisha mazingira ya viwanda vya uchakataji gesi yanatunzwa, mfano, mabaki ya majimaji yanayotokana na uchakataji wa gesi yanachujwa na kuteketezwa inavyostahili, pia kuhakikisha hakuna kelele zinazosumbua wananchi wanaoishi maeneo ya jirani na kiwanda.

“Pia EWURA itahakikisha hakuna athari zitakazotokea katika ardhi, kama mmomonyoko wa udongo unaoweza kutokea kwasababu ya kupitisha mabomba ya kusafirisha gesi pia kuhakikisha wananchi wanaishi umbali uliokubalika kutoka katika miundombinu hiyo inapopita ili kuwakinga na maafa mbalimbali yanayoweza kutokea mfano, ajali za moto na nyingine zinazoweza kusababishwa na kuvuja kwa gesi hiyo”

Kwa kumalizia na sekta ya maji na usafi wa mazingira, Bwana Kaguho alisema, EWURA imekuwa ikihakikisha mamlaka za maji zinatoa huduma ya maji safi na taka inayoendana na viwango vilivyowekwa na TBS.



Meneja wa EWURA wa Kanda ya Ziwa, Mha. Nyirabu Musira akitoa ufafanuzi kwa wageni mbalimbali waliotembelea banda la EWURA wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani yaliyofanyika Juni 2017, Butiama, Mkoa wa Mara.

Mamlaka za maji zinapaswa kupitia ukaguzi na uchunguzi juu ya athari za mazingira zinazoweza kusababishwa na miradi mipya pamoja na miradi iliyopo na ikithibitika kukidhi viwango, Mamlaka hiyo inapata cheti kutoka baraza la taifa la mazingira NEMC.

Mapema mwezi Juni Mwaka huu, EWURA kanda ya Ziwa ikiongozwa na Meneja wa Kanda hiyo Mhandisi Nyirabu Musira, ilishiriki katika maadhimisho ya siku ya mazingira duniani, iliyofanyika kitaifa Wilayani Butiama mkoa wa Mara, ili kuelimisha umma, jinsi shughuli za sekta zinazodhibitiwa zinavyoweza kufanyika bila kuharibu mazingira. Maadhimisho ya Siku

ya Mazingira yaliandaliwa na Ofisi ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Raisi (Muungano na Mazingira) chini ya Waziri wake Mheshimiwa January Makamba na kufungwa na Makamu wa Raisi wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu ambaye alisisitiza utunzaji wa Mazingira kwa maendeleo ya viwanda nchini.

EWURA Kanda ya Ziwa ilishishiki maadhimisho hayo kwa kushiriki kwenye maonesho pamoja na midaharo mbalimbali iliyoendesha juu ya utunzaji wa mazingira, ikisindikizwa na kauli mbiu isemayo **“Hifadhi ya Mazingira: Muhimili wa Tanzania ya viwanda”**

Wawakilishi Zanzibar waitembelea EWURA kujifunza udhibiti

Na Wilfred Mwakalosi

Kamati ya Ardhi na Mawasiliano ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar limesifu jitihada na mafanikio ya Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) katika masuala ya udhibiti, na kwamba Zanzibar pia ingependa kuona taasisi yake ya udhibiti wa huduma (ZURA) ikibadilika na kuwa kwenye viwango vya EWURA.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Abdulkarim Esmail Hassan Shah aliomba EWURA kuisaidia ZURA kiutaalam, ili iweze kuwa katika viwango vinavyotakiwa katika kutoa huduma.

“ZURA ni taasisi mpya, tunafikiria kwamba, ushirikiano wa karibu kati ya taasisi hizi mbili utasaidia kuleta matunda yanayostahili hasa kwenye eneo la kuongeza uwezo wa kitaalam,” alisema.

Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira Juma Makungu Juma alisema wakati wa ziara hiyo kwamba, Wizara yake itafanya kila iwezavyo kuhakikisha kwamba ZURA inapata msaada unaotakiwa ili kuiinua ifikie viwango vinavyotakiwa.

“Tunajivunia sana EWURA. Tungetamani mkafanye udhibiti hata Zanzibar, hasa wa mafuta, ili kuweka nidhamu,” alisema. Hata hivyo, EWURA ina uwezo wa kisheria wa kufanya kazi Tanzania bara tu.

EWURA hata hivyo imekuwa ikifanya kazi kwa karibu sana na ZURA kwa miaka mitatu iliyopita, ikiisaidia tangu mipango ya awali kabisa ya kuanza kwake, kuhakikisha kwamba inapata uzoefu unaotakiwa. Kamati hiyo ya Baraza la Wawakilishi iliitembelea EWURA ili kujifunza namna ambavyo shughuli za udhibiti zinafanywa. Kamati pia ilipata fursa ya kushuhudia ukaguzi wa vinasaba kwenye mafuta ja petroli, ikiwa njia mojawapo ya kudhibiti ubora wa mafuta hayo. Kaimu Mkurugenzi wa EWURA Mhandisi Godwin Samwel alisema, ofisi yake imekuwa ikitoa msaada wa kiufundi kwa ZURA ili kuhakikisha kwamba Mamlaka hiyo mpya inaanza kwa hatua sahihi.

“Mlango wa EWURA siku zote utakuwa wazi kwa ndugu zetu wa visiwani ili kuhakikisha kwamba taasisi hizi mbili zinafanya kazi pamoja kwa manufaa ya nchi yetu,” alisema.



Baadhi ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Watendaji wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar wakati wa ziara ya mafunzo kuhusu masuala ya udhibiti, iliyofanyika mwezi Agosti 2017, makao makuu ya EWURA, Dar es Salaam.

EWURA kwenda *kidijitali*

Na Tobietha Makafu

Kuanzia tarehe moja ya mwezi wa nane mwaka 2016 EWURA imeanza rasmi kutumia mfumo mpya wa kielektroniki kwa maombi yote ya leseni za ukandarasi wa umeme, uzalishaji na usambazaji wa umeme pamoja na maombi ya bei kwa sekta ya maji, malalamiko na taarifa.

Hivyo yeyote anayehitaji kufanya maombi ya leseni hizo ni lazima atume maombi kwa njia ya mtandao kwa kutumia mfumo unaoitwa Licensing and Order Information System (Mfumo wa leseni na Maamuzi (LOIS) ulioanzishwa na EWURA kwa kupitia tovuti ya <https://lois.ewura.go.tz>.

Mfumo huu wa LOIS unatumika kuboresha utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya EWURA ambayo ni kutoa, kudurusu na kufuta leseni, kudhibiti bei na tozo, kufuatilia ufanisi wa utendaji wa sekta zinazodhibitiwa, kusikiliza malalamiko na kutatua migogoro.

Akizungumza na mwandishi wa habari hii Meneja Mawasiliano na Uhusiano EWURA, Bw. Titus Kaguo alisema, Lengo la kutumia njia ya mtandao kutuma maombi ya leseni ni kupunguza muda wa upatikanaji wa leseni hizo zinazotolewa na EWURA, pia kuwawezesha waombaji kupata taarifa na kufuatilia hatua za utekelezaji wa maombi yao moja kwa moja katika mfumo huo.

“Mfumo huu mpya unatarajiwa kurahisisha mawasiliano kati ya idara moja na nyingine pia mawasiliano kati ya EWURA na wadau wengine, katika kurahisisha utoaji wa huduma za leseni, maombi ya bei na tozo pamoja na kusaidia mawasiliano ndani ya mamlaka” alisema.

Ufanisi wa utoaji huduma utaongezeka kwa kuongeza uwazi wa mchakato wa utoaji huduma za EWURA kwa wateja, ambapo wateja

wataweza kutuma maombi na kuona hatua iliyofikiwa kwa maombi waliyowasilisha EWURA kwa kutumia mtandao wa intaneti. Hivyo mteja hatalazimika kufika ofisi za EWURA ili kuwasilisha maombi ya huduma mbalimbali zinazotolewa.

Akieleza jinsi ya kutumia mfumo huu alisema, mfumo huu wa Leseni na maagizo (LOIS) unapatikana katika tovuti ya EWURA www.ewura.go.tz, mteja atatakiwa kujisajili ili kuweza kutumia mfumo huu. Baada ya kujaza fomu ya maombi au kuwasilisha malalamiko atapokea ujumbe unaoeleza kuwa maombi yake yamepokelewa.

“Mfumo huu mpya unatarajiwa kurahisisha mawasiliano kati ya idara moja na nyingine pia mawasiliano kati ya EWURA na wadau wengine, katika kurahisisha utoaji wa huduma za leseni,
- Titus Kaguo

Ikiwa EWURA itaona kuna haja mteja kuwasilisha taarifa nyingine au kutoa ufafanuzi, maagizo haya yatatumwa moja kwa moja kwa mteja kupitia mfumo huu. Mara maombi yakipitishwa mteja atapata taarifa kwa kupitia mfumo huu.

Baada ya maombi kukamilika, mchakato wa ndani utaendelea kama kawaida hadi hatua ya Bodi ya EWURA kupitisha maombi ya mteja.

Mfumo wa LOIS umeandaliwa kwa kuzingatia mahitaji ya EWURA na wadau. EWURA ipo tayari kupokea maoni kuhusu mfumo huu kupitia anuani zake na ofisi zake za makao makuu au ofisi za kanda zilizopo mikoa ya Mwanza, Arusha, Mbeya na Dodoma.

Muongo mmoja wa **EWURA** kuchapa kazi, yapanua wigo wa huduma, yaimarisha viwango

Na Asiatu Msuya

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (EWURA) ni Taasisi ya Udhibiti wa huduma za sekta mtambuka iliyoundwa kwa Sheria EWURA, Ukurasa wa 414 ya Sheria za Tanzania. EWURA ilianza rasmi mwaka 2006, baada ya miaka minne ya maandalizi ya kuanzishwa kwake. Na hatimaye mwaka 2016, Mamlaka ilitimiza miaka kumi ya utoaji huduma za kiudhibiti, yaani muongo mmoja.

Shughuli kuu za Mamlaka ni pamoja na kudhibiti sekta za Nishati na Maji Tanzania Bara. EWURA ina wajibu wa kuzidhibiti sekta hizi kiufundi na kiuchumi. Sekta ndogo zinazothibitiwa na Mamlaka ni Petroli, Gesi Asilia, Umeme na Maji na Usafi wa Mazingira.

Mamlaka inao wajibu wa kuhakikisha kuwa huduma hizi zinapatikana kwa viwango vya hali ya juu, kwa bei nafuu, salama na kwa uhakika, na kwamba watoa huduma wanapata faida ya haki kwenye vitega uchumi vyao.

Utekelezaji wa majukumu na wajibu wa EWURA

Katika kutekeleza wajibu na kazi zake, EWURA imenuia na kuwiwa kuboresha hali ya jamii ya Watanzania kwa kuchochea ushindani na ubora wa kiuchumi; Kulinda maslahi ya wataji; Kulinda uimara wa kifedha wa watoa huduma; Kuchochea upatikanaji wa huduma zinazothibitiwa na Kulinda na kutunza mazingira.

Ili kutekeleza majukumu na wajibu wake kwa uwazi na katika namna yenye manufaa kwa wote, EWURA inafuata sera za Kisekta, Sheria kuu na miongozo na kanuni mbalimbali zinazotolewa na Mamlaka.

Sera na Sheria zinazosimamia utekelezaji wa majukumu ya EWURA ni pamoja na Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (2001), Sheria ya Umeme (2008), Sheria ya Petroli (2015) na Sheria ya DAWASA sura ya 273.

Wigo wa Upatikanaji huduma za EWURA

Katika kutekeleza majukumu yake ya Udhibiti nchini, EWURA imepanua wigo wake ndani ya kipindi cha miaka 10 tangu kuanzishwa kwake; kutokana na nguvu na mikakati thabiti iliyowekwa katika kujenga uwezo, kuimarisha utendaji kazi na kuboresha viwango vya utoaji huduma.

Kutanabahisha hilo, EWURA imeweza kuanzisha Ofisi za Kanda katika mkoa wa Arusha; kwa Kanda ya Kaskazini, mkoa wa Mbeya kwa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini; mkoa wa Mwanza kwa Kanda ya Ziwa na mkoa wa Dodoma kwa Kanda ya Kati ambapo pia ndio patakapokuwa makao makuu ya Ofisi za EWURA.

Lengo la kupanua wigo wa huduma za Udhibiti ni kusaidia kusogeza huduma za na kutatua changamoto zinazowakumba watoa huduma



na wananchi; ambapo awali huduma hizo zilikuwa zikipatikana Dar es Salaam pekee.

Viwango vya Utoaji Huduma za EWURA

Katika kuhakikisha kuwa EWURA inaishi dira yake inayosimamia katika kutoa huduma za kiwango cha kimataifa; utoaji huduma za udhibiti za Mamlaka unapimwa kwa viwango maalumu vya kimataifa kwa minajili ya kuhakikisha kuwa huduma zitolewazo zinapatikana kwa bei nafuu, salama na kwa uhakika. Kwa muktadha

huo, EWURA imepimwa na kufuzu viwango vya Shirika la Kimataifa linalodhibiti viwango vya utoaji huduma yaani ISO ili kuhakikisha kuwa huduma zake zinakuwa na ubora unaotambulika kimataifa kwa lengo la kumlinda mtumiaji wa huduma hizo ambaye ni mwananchi wa kawaida anayetumia huduma za maji, umeme, gesi na petroli.

Mamlaka imefanikiwa kwa kiwango kikubwa katika kuzingatia viwango ilivyojiwekea na katika kutimiza vigezo vya ubora vya ISO, na hivyo kupelekea kupewa cheti cha ubora cha ISO: 9001:2008.

Matumizi sahihi na salama ya **GESI YA KUPIKIA** majumbani



Na Tobietha Makafu

Gesi ya kupikia majumbani, kitaalamu LPG (Liquefied Petroleum Gas) ni gesi inayotumika majumbani kwaajili ya kupikia.

Gesi hii ni zao la petroli inayopatikana kwa kusafishwa kwa mafuta ghafi, ni nishati iliyo rafiki kwa mazingira inayopatikana kwa uhakika na bei nafuu hivyo kupelekea watu wengi duniani kuitumia.

Gesi hii ya kupikia majumbani hutofautiana kikemikali na gesi asilia (Natural Gas) kwa sababu, gesi asilia inaundwa na kemikali ya Methane huku gesi ya kupikia inaundwa na Propane na Butane. Hii haimaanishi kuwa gesi asilia haiwezi kutumika kupikia nyumbani lakini yenyewe inahitaji mtandao wa mabomba na si rahisi kuiweka kwenye mtungi kama LPG.

Ili gesi hii itumike kwa usalama na inavyopaswa, mtumiaji anapaswa kuzingatia hatua za kiusalama kwaajili ya kulinda afya pamoja na mazingira kwa ujumla.

Moja ya vitu vya kwanza kabisa mtumiaji anatakiwa kuzingatia ni pamoja na kununua gesi iliyopo kwenye mtungi wenye lakiri ya kampuni husika na lakiri hiyo isiwe imevunjwa ama kuharibiwa na ahakikishe ana pima uzito wa mtungi wa gesi aliyonunua ili kujiridhisha na uzito wa gesi hiyo.

Gesi inapaswa kusafirishwa ikiwa imesimama wima na ihifadhiwe katika eneo lenye hewa ya kutosha na ikae mbali na vyanzo vyovyote vya moto. Endapo mtumiaji atagundua kuna uvujaji wa gesi, lazima asiwashe jiko kama alikua hajaliwasha, zima jiko kama lilikuwa linatumika, ondoa "regulator" ya gesi iliyoko kwenye mtungi.

Ikiwa mtungi utaendelea kuvuja, uondoe na uuweke sehemu ambayo ni salama mbali na mitungi mingine kama ipo, usiwashe wala kuzima kifaa chochote cha umeme kwani kufanya hivyo kutasababisha muwako wa mara moja na usitumie simu ya mkononi wakati upo katika eneo hilo.

Wakati wa kutumia gesi hii ni muhimu kufungua milango au madirisha. Hakikisha unatumia hozi inayotakiwa na haijajikunja ili kuzuia mbinyo na kusababisha kuharibika. Vile vile mtumiaji anatakiwa ahakikishe mitungi imetunzwa mbali ambapo si rahisi kugongwa au kuangukiwa na kitu chochote.

Si watumiaji tu wa LPG wanaotakiwa kuzingatia hatua za usalama kuhusu gesi hiyo bali hata wafanya biashara hususani wale waagizaji wa jumla, na wasambazaji wakubwa lazima wazingatie misingi ya usalama na viwango. Lengo kubwa likiwa ni kukidhi usalama wa watu na mali zao pamoja na mazingira kwa ujumla.

EWURA yawafunda waajiriwa wapya

Na Mwandishi wetu

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imeendelea kuwajengea uwezo watumishi wake, wakiwemo watumishi wapya wanaojiunga na Mamlaka kwa lengo la kuwafunda na kuwapa nyenzo za kufanyia kazi; zitakazowaongoza punde tu wanapoanza kutekeleza majukumu yao.

Mafunzo kwa waajiriwa wapya yanaandaliwa mahsusi ili kuwawezesha kuelewa taratibu za utendaji kazi za Mamlaka na kazi mbalimbali za Udhibiti zinaotekelezwa na EWURA kila siku.

Mafunzo haya mahsusi yaliyofanyika mwezi Agosti, 2017 katika Ofisi za EWURA zilizopo Dar es Salaam, yalijumuisha waajiriwa wapya 20 wa kada za Uhandisi, Wakaguzi wa mifumo ya utendaji kazi ya umeme na Petroli, Uhasibu, Mawasiliano na Uhusiano na Utawala na Usimamizi wa Ofisi.

EWURA iliandaa mafunzo haya ya awali kwa waajiriwa wapya ikiwa ni njia ya kuwawezesha waajiriwa hao kuelewa tamaduni za mahali pao pa kazi, ili waweze kulandana na miiko na tabia za Mamlaka katika kuhudumia wateja wake; kujifunza namna sahihi ya kutekeleza majukumu kwa mujibu wa Sheria, miongozo na kanuni zilizopo; na kuwafanya waajiriwa wapya kuijua Mamlaka ipasavyo ili kumudu utekelezaji wa wajibu wa kiudhibiti, na kujiimarisha kiutendaji na kitaaluma wakati wa kipindi cha mpito cha ili kuweza kutoa huduma stahiki katika kuwahudumia wateja wa Mamlaka katika nyanya mbalimbali. Wakati akiwakaribisha waajiriwa wapya.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Mhandisi Godwin Samwel alieleza kuwa: “EWURA Taasisi inayodhibiti sekta mtambuka na kwayo imejiwekea dira ya kutoa huduma za udhibiti wa nishati na maji kwa kiwango cha kimataifa, na kwa mantiki hiyo inampasa kila mwajiriwa wa Mamlaka kuzingatia miongozo na kanuni za utendaji kazi zilizowekwa ili kufikia viwango vya huduma vinavyostahili wakati wowote anapotoa huduma kwa niaba ya Mamlaka”.

Mhandisi Godwin ametumia nafasi hiyo kuwaomba watumishi wote wa EWURA kuunga mkono juhudi zinazofanywa na Mamlaka katika kuimarisha uwezo na viwango vya utendaji kazi, ambapo ameeleza kuwa, pamoja na mafanikio makubwa ambayo yamefikwa katika utoaji wa huduma na utekelezaji wa majukumu yake, Mamlaka bado inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo maelekezo ya Serikali ya mara kwa mara ambayo mara nyingine yanaweza kukinzana na miongozo ya utendaji kazi wa Mamlaka, au kusababisha ucheleweshaji katika kutoa uamuzi wa hivyo kuwataka watumishi kuelewa changamoto hizo na kuzitafutia ufumbuzi wa pamoja.

Aidha, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, amewasisitiza waajiriwa wapya kuhakikisha kuwa wanawapatia huduma wateja wa Mamlaka kwa uwazi, na kwa viwango vya kutosha, salama na kwa uhakika na kwamba watoa huduma wanapata faida kwenye vitega uchumi vyao ili hatimaye huduma zinazotolewa ziweze kuwa na mchango chanya katika jamii na maendeleo ya Taifa kwa ujumla.

Mikoa ya Kaskazini kupokea mafuta Bandari ya Tanga

Na Asiatu Msuya

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (EWURA), imetangaza uamuzi wa kuanza kutumia Bandari ya Tanga kupokelea mafuta ya petroli kwa mikoa ya Tanga, Arusha, Kilimanjaro na Manyara, ifikapo Oktoba 2017; ili kuongeza usalama wa upokeaji wa mafuta nchini, hasa pale itakapotokea bandari ya Dar es Salaam kutoweza kupokea mafuta hayo kwa sababu mbalimbali.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (EWURA), Mha. Godwin Samwel, ametoa uamuzi huo Agosti 24, 2017 Mkoani Tanga, katika kikao cha pamoja kati ya EWURA, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na wadau mbalimbali kutoka makampuni yanayofanya biashara ya mafuta (OMC's) ambapo ameeleza kuwa; hatua hiyo imefikwa ikiwa ni utekelezaji wa azimio la Serikali kuhusu kuanza tena kupokea mafuta ya petroli kupitia Bandari ya Tanga, baada ya kusitishwa kufanya hivyo kwa miaka kadhaa kabla.

Eng. Samuel ameongeza kuwa, Serikali ilipitisha azimio hilo, ili kuongeza idadi za bandari zinazopokea mafuta ya petrol nchini, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kua, wananchi wa Mkoa wa Tanga na Mikoa ya Kaskazini, wanapata mafuta ya bei nafuu kutokana na kupungua kwa gharama ya kuyafirisha mafuta hayo kutoka Dar es Salaam; ikizingatiwa kua, bei kikomo za mafuta katika mikoa hii zitakuwa zikipangwa kutoka Tanga.

Katika kutekeleza azimio hili, Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (EWURA) ilifanya tathmini na kujiridhirisha kuimarika na kukidhi ubora kwa miundombinu ya ghala (depot/terminal) la kampuni ya mafuta ya GBP Tanzania (GBP), kwa ajili ya kupokea na kuhifadhi mafuta kutoka kwenye meli za BPS ambapo uwezo wa ghala hilo umefikia lita zaidi ya 120 milioni kwa

mafuta ya aina ya petroli, dizeli na mafuta ya taa; kutoka lita 20 milioni Julai 2015.

Aidha, mahitaji na matumizi ya mafuta katika Mkoa wa Tanga na Mikoa ya Kaskazini inakadiriwa kuwa kiasi kisichozidi lita 35 milioni kwa mwezi. Kwa mantiki hiyo, kwa uwezo wa sasa wa kupokea lita zaidi ya milioni 120 kwa ghala la GBP na pia uwezo wa kupakia maloli yasiyopungua 50 (lita zaidi ya milioni 1.5) kwa siku, ni dhahiri, kuwa ghala hili linaweza kupokea mafuta kwa ajili ya Mikoa ya Kaskazini na Mkoa wa Tanga wenyewe bila shida yeyote. Mpaka sasa, GBP ndiyo inayomiliki miundo yote ya kupokelea mafuta katika bandari ya Tanga ikiwa ni pamoja na gati (jetty) na bomba la kupokelea kutoka kwenye meli mpaka kwenye matenki, hivyo EWURA inazishauri kampuni zingine (hasa zile zilizokuwa na maghala za mafuta (OMCs) kujenga maghala zaidi ya kupokelea na kuhifadhi mafuta ya BPS mjini Tanga ili kushamirisha ushindani katika utoaji wa huduma ya kupokea na kuhifadhi mafuta ya petroli.

Hata hivyo, EWURA itaendelea kufuatilia kwa karibu sana (kupitia masharti maalumu ya leseni aliyopewa GBP) utendaji wa kampuni ya GBP, hasa inavyotoa huduma kwa wateja na washindani wenzake wanaotumia ghala la GBP Tanga kupokelea na kuhifadhi mafuta yao, ili kuhakikisha kua huduma zinazotolewa zinazingatia usawa na ushindani unaotarajiwa na kuchukua hatua muafaka pale inapobainika mapungufu.



Ghala la kuhifadhi mafuta la GBP - Tanga

Ewura yang'ara Maonesho ya Sabasaba

Na Tobietha Makafu

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imefanya vizuri katika maonesho ya 41 ya kimataifa ya biashara ya sabasaba yaliyofanyika katika viwanja vya Mwalimu Nyerere, vilivyopo jijini Dar es Salaam kuanzia 28 Juni mpaka 13 Julai.

Katika maonesho ya mwaka huu EWURA imefanikiwa kuibuka mshindi wa tatu katika kundi la Nishati na Madini, kundi ambalo lilishirikisha taasisi na kampuni binafsi na zile za serikali zinazojihusisha na utoaji huduma na bidhaa katika sekta ya Nishati na Madini nchini.

Ushindi huo ulichangiwa na maandalizi bora yaliyozingatia vigezo na masharti ya ushiriki pamoja na utoaji huduma bora kwa wateja waliotembelea banda la EWURA kwa ujumla.

Aidha wataalamu wa taasisi hii wamekua wakitoa elimu ya kina kuhusu huduma za taasisi katika sekta zinazodhibitiwa ikiwa ni pamoja na kutatua changamoto na malalamiko ya wateja yanayohusu huduma zitoilewazo.

Meneja Mawasiliano na Uhusiano Bw. Titus Kaguho alisema, watu mbalimbali walitembelea



Baadhi ya wageni wakisikiliza kwa makini maelezo kutoka kwa maofisa wa EWURA walipotembelea banda la EWURA katika Maonesho ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF - Sabasaba).

banda la EWURA msimu huu, wakiwa na lengo la kujionea na kujifunza kuhusu huduma mbalimbali zitolewazo, kupata elimu na majibu ya maswali mbalimbali yahasuyo mamlaka katika sekta ya Nishati (Umeme, Petroli na Gesi asilia) pamoja na sekta nzima ya maji.

“Tumepokea watu wengi kwa siku waliovutiwa na banda letu wakitaka kufahamu zaidi kuhusiana na huduma mbalimbali zinazotolewa na EWURA katika sekta zote tatu inazodhibiti.

Aliongeza kuwa, mbali na huduma zitolewazo watembeleaji wa banda walionekana kuvutiwa na kufurahishwa uwepo wa ripoti mbalimbali za sekta ya petrol na maji, ambapo wanafunzi, watafiti pamoja na wananchi waliohitaji walipatiwa repoti hizo ili zivasaidie katika shughuli zao mbalimbali za kujenga nchi. Nao wateja waliofika kwenye banda hilo walionekana kuridhishwa na kuvutiwa kwa kiasi kikubwa na maelezo pamoja na huduma walizopata katika banda hilo la EWURA.

“Kwakweli elimu niliyoipata imeondoa mkanganyiko uliokupeo kichwani mwangu mwanzoni kuhusu EWURA, kazi na wajibu wake, pia nimefahamu namna bora ya kuwasilisha malalamiko yangu juu ya sekta mnazodhibiti EWURA.

Anabainisha mkazi wa jiji aliyejitambulisha kwa jina la Mariam Saidi.

“Kwakweli elimu niliyoipata imeondoa mkanganyiko uliokupeo kichwani mwangu mwanzoni kuhusu EWURA, kazi na wajibu wake, pia nimefahamu namna bora ya kuwasilisha malalamiko yangu juu ya sekta mnazodhibiti EWURA. Anabainisha mkazi wa jiji aliyejitambulisha kwa jina la Mariam Saidi.

Katika kutimiza wajibu wake wa kutoa elimu kwa umma, EWURA itaendelea kushiriki katika maonesho mbalimbali yatakayofanyika nchini ili kuwafikia wananchi wengi Zaidi katika maeneo mbalimbali.

Hivyo EWURA inapenda kuwakaribisha wananchi wote kutembelea banda lake katika maonesho mbalimbali yatakayofanyika nchini. Pia EWURA inawakaribisha wananchi kutembelea ofisi zake ya makao makuu iliyopo jijini Dar es Salaam na zile za kanda ambazo zipo Kanda ya Ziwa mkoani Mwanza, Kanda ya Kaskazini iliyopo Mkoani Arusha pamoja na Ofisi za Kanda ya Nyanda za Juu kusini Mkoa wa Mbeya ili kujipatia ufafanuzi wa masuala mbalimbali kuhusu udhibiti wa Nishati na Maji.



Maofisa wa EWURA, Bi. Rabel Kiula (Kulia) na Mha. Violet Iramu wakisikiliza kwa makini wageni waliotembelea banda la EWURA katika Maonesho ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF - Sabasaba).